# GEREZA LA HAZWA

## UTANGULIZI

**Wakati nyie mnalala mkiwa mnausaka usingizi wa pono, watu wenye ndoto zao ambao wanaiogopa njaa kuliko kitu chochote kile wapo macho kuzitafuta na kuzisaka ndoto zao kuhakikisha mwanaharamu ambaye anaitwa tumbo anaridhika kwa namna yoyote hata kwa kumlazimisha.**

**Ni wanadamu ambao wanaamini mikono yao ndiyo msaada wao wa pekee wa kuweza kuendelea kuwa hai na kupunguza mateso pamoja na**

**dhihaka za kuchekwa na wanadamu wasiokuwa na uoga wowote mbele ya dunia ya muumba. Hao ndio watu ambao wanaweza kuiishi hii dunia yenye kila aina ya vioja vya ajabu na vya kutisha pia.**

**Kwao hawaamini katika bahati, juhudi kwanza ndizo zinazo wapa imani ya kujikwamua kwenye maisha magumu ambayo wanayapitia wakiamini hakuna kitu kirahisi kukipata kwenye ulimwengu, ni lazima ulipie ndipo ukipate unacho kitaka na hawana pesa wanafanyaje? Basi jasho lao ndiyo malipo ambayo**

wanatakiwa kuyalipa matumbo ili tu wafanikishe moja ya ndoto zao za kuwa na maisha ya angalau kupata hata milo miwili mpaka mitatu kwa siku.

"The bright future is only for the brave" ni kauli ambayo inawapa muongozo wa nini wanatakiwa kukifanya kwenye maisha yao kama tu watahitaji kuipata ahueni ya maisha huku wakiamini ujasiri wao na ushujaa wao ndicho kitawapa kesho iliyo njema. Hawana mashamba ya kusema wajifariji kwamba kama wakitaka mali basi wataipata

**shambani, hivyo nguvu zao ndio mtaji wao. Yes, hayo ndiyo maisha halisi kwao.**

# SURA YA KWANZA

# MAISHA YANGU NI KIFO

## *ARUSHA, TANZANIA*

**Ndani ya machimbo ya moja ya madini adimu zaidi ulimwenguni (Tanzanite) yanayopatikana ndani ya nchi moja tu ulimwengu mzima ambayo ni Tanzania, kuna wanaume walikuwa wapo ndani kabisa sehemu ambayo ilikuwa na kiza cha kutosha. Tochi zilizofungwa kwenye vichwa vyao zilikuwa ni sehemu ya**

kuwasaidia kuona vitu ambavyo vilikuwa mbele yao.

Sio kwamba walikuwa sehemu ambayo haina umeme kiasi kwamba wakashindwa kuona nini kilichopo huko, hapana! Bali ni moja ya njia za kuweza kuzisaka na kuzifikia ndoto zao, walikuwa wapo mgodini ndani kabisa ambako hata mwanga wa jua huwa ni ndoto kuonekana, mtu anakuwa kama yupo dunia ya peke yake tofauti na hii dunia ya kawaida ambayo kila mwanadamu anaiishi.

Kama mtu angeshtuka kutoka usingizini akajikuta hiyo sehemu

**angehisi kwamba ulikuwa usiku wa manane kulingana na aina ya kiza kizito ambacho kilitanda ila ni muda ambao usingeamini kama ilikuwa ni jioni ya kawaida kwenye dunia ya huku nje ambayo watu walikuwa wanaendelea na shughuli zao za kila siku hasa kwa wale wasaka tonge na wengine ambao kwao kazi ni mwiba uwachomao hawakuacha kuendelea kupiga majungu na jingi kwenye vijiwe mbalimbali na kuendelea kuzijutia zamani zao badala ya kuziwaza na kuzijenga kesho zao ziliyo bora.**

Ndani ya mgodi ambao unajulikana kwa kuwa na madini ya Tanzanite ndimo walimo onekana wanaume wa kazi wakiwa hawaongei ila vitendo vyao vilijionyesha. Majembe mazito, uma, nyundo na machepeo ndivyo vitu vilivyo ongea zaidi huko, wanaume walikuwa hawalali kuhakikisha maisha bora yanakuja kupitia imani zao za ufanyaji kazi kwa bidii.

Vijana zaidi ya watano kila mmoja akiwa upande wake, walikuwa wanapambania kombe chini ya ardhi ambako kama ingetokea namna

**yoyote kukajifunika basi hadithi zao zingekuwa zimeishia huko huko chini ila hakukuwa na namna wangeweza kuyafanya maisha yakawa malaini kwao kwa mlo wao wa siku moja kwa siku zaidi ya kujitoa mhanga. Ilikuwa ni zaidi ya masaa matano wakiwa wanafanya kazi kwa bidii.**

**Unahisi kuna nini nyuma ya maisha ya hawa vijana? Huyu mwanaume wa kuitwa Alen ni nani? Ana nini nyuma yake? Kuna maandiko ya siri yalikuwa yanadai kwamba yeye alikuwa ni moja kati ya viumbe hatari zaidi kuwahi kutengenezwa kwenye ulimwengu huu.**

**Huyu bwana alidaiwa kuhusika na mauaji ya watu 150 wakiwemo makomando hatari 33 hivyo akawa anatafutwa na nchi za Afrika ya**

**Magharibi na Kaskazini kuliko hata pesa ilivyokuwa inatafutwa.**

**Sasa iliwezekanaje mtu kama huyo kuja kuishia kwenye machimbo huko Arusha tena akionekana kuwa mtu wa kawaida kabisa mtaani?**

**Karibu uweze kukisoma kitabu bora zaidi cha kijasusi kuwahi kuandikwa kwenye ardhi ya Tanzania ambacho kinaitwa GEREZA LA HAZWA. Karibu tuungane kwa Pamoja kuzifunua kurasa hizi ndani ya hilo gereza la Hazwa.**

**Mwandishi jina langu naitwa FEBIANI BABUYA**

**WhatsApp: +255621567672**

**Email: thomasibabuya@gmail.com**